



## Utangulizi wa Mhariri: Mitazamo ya Fasihi Afrika Mashariki

Ken Walibora Waliaula

**To cite this article:** Ken Walibora Waliaula (2019) Utangulizi wa Mhariri: Mitazamo ya Fasihi Afrika Mashariki, *Eastern African Literary and Cultural Studies*, 5:3-4, 151-154, DOI: [10.1080/23277408.2019.1620978](https://doi.org/10.1080/23277408.2019.1620978)

**To link to this article:** <https://doi.org/10.1080/23277408.2019.1620978>



Published online: 25 Nov 2019.



Submit your article to this journal [↗](#)



Article views: 2979



View related articles [↗](#)



View Crossmark data [↗](#)



## Utangulizi wa Mhariri: Mitazamo ya Fasihi Afrika Mashariki

Ken Walibora Waliaula

Global and Language Studies Centre, Department of International Relations and Diplomacy, Riara University, Nairobi, Kenya

**Keywords** Fasihi; Upya; Uhakiki; Mitazamo; Afrika Mashariki

Hili toleo maalum la jarida la *East African Literary and Cultural Studies*, sio tu kwamba ni la kihistoria tu bali limetokea wakati mwafaka katika historia ya maendeleo ya Kiswahili. Kumekuwa na mwamko mpya kuhusiana na maendeleo ya Kiswahili ndani na nje ya Afrika Mashariki, mwamko ambao ni mwanngwi wa mawanio na matarajio ya wakereketwa wa Kiswahili wa tangu azali. Baba wa fasihi ya kisasa ya Kiswahili Shaaban bin Robert au kwa jina jingine Shaaban Ulenge, alikuwa miongoni mwa wachangiaji wakubwa wa fasihi ya Kiswahili na utetezi wa lugha hii ya mawasiliano mapana katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Katika kuingia upatu lugha hii Robert anatumia methali ya Kiswahili inayosema; “Titi la mama litamu japokuwa la mbwa” kama nguzo ya shairi lake la “Kiswahili.” Anasema:

Lugha kama Kiarabu, Kirumi na Kingereza  
Kwa wingi zimeratibu, mambo ya kupendeza  
Na mimi nimejaribu, kwa kila hali kujifunza  
Lakini sawa na bubu, nikizisema nabezwa  
Titi la mama litamu, jingine halishi hamu.

(Robert 1966:27)

Kutolewa kwa toleo maalum la jarida hili la EACLS kwa lugha ya Kiswahili ni hatua muhimu katika sio kuitambua lugha hii na fasihi yake bali pia katika kutambua hatua zilizowahi kufikiwa katika mawanda mbalimbali hasa baada ya uhuru.

Ukuzi wa Kiswahili umekuwa mkubwa kihistoria hususan katika nchi za Kenya na Tanzania ambako kilitumika pakubwa katika kuwahamasisha na kuwaunganisha wenyeji katika harakati za ukombozi kutoka kwa minyororo ya Wakoloni. Katika nchi hizi mbili matumizi ya Kiswahili kama lugha ya taifa yamekuwapo kwa muda mrefu, si hoja kama matumizi hayo yametokea baada ya tamko rasmi ama la kikatiba au la. Ila katika miaka ya hivi karibuni mataifa mengine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAM) yamejikuta hayana budi kukweza hadhi ya lugha hiyo katika mitagusano ya ndani na nje ya mipaka ya nchi. Mwafaka ulioweka msingi wa kuundwa kwa JAM unasema kwamba Kiswahili

ndiyo lugha ya mawasiliano mapana kwa nchi zote wanachama ikiwa ni pamoja na Uganda, Burundi, Rwanda, na Sudan Kusini, mbali na zile mbili za awali. Aidha Bunge la Afrika Mashariki limekwishapitisha kwamba Kiswahili kitumike kama lugha rasmi ya Jumuiya. Azimio hilo limetokea zaidi ya mwongo mmoja tangu Umoja wa Afrika ulipokipitisha Kiswahili kuwa mojawapo ya lugha zake rasmi kando na Kireno, Kiarabu, Kiingereza, na Kifaransa. Isitoshe, JAM imebuni Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA), chombo mahsusi chenye makao yake makuu Zanzibar na ambacho kimejukumishwa kuelekeza na kuendeleza ukuzaji wa Kiswahili ndani ya ukanda wa Afrika Mashariki.

Kukwezwa kwa hadhi na matumizi ya Kiswahili Afrika Mashariki kunamaanisha sio tu kwamba Kiswahili kinafundishwa na kitafundishwa katika eneo zima, bali fasihi yake inapata umuhimu mkubwa. Huku kufundishwa kwa Kiswahili kwa miaka na mikaka kumechangamkiwa na mataifa mengine nje ya Afrika Mashariki na hali kadhalika nje ya Afrika. Mathalan tangu nyakati za vita baridi kati ya Marekani na Muungano wa Sovieti, Kiswahili kimefundishwa katika nchi mbalimbali katika pande mbili za mirengo hiyo miwili. Na hata baada ya kukoma kwa vita baridi kufuatia kusambaratika kwa Muungano wa Sovieti, bado Kiswahili ni kivutio kikubwa katika taasisi za elimu katika mataifa kama vile Urusi, Ujerumani, Ujapani, Uchina, Austria, Kanada, Uingereza, Marekani na Meksiko. Barani Afrika lakini nje ya Afrika Mashariki mataifa kama vile Ghana, Naijeria, na Misri yamekuwa na historia ndefu ya ufundishaji wa Kiswahili na fasihi yake katika viwango tofauti tofauti. Hivi karibuni zaidi, msisimko huu kukielekea Kiswahili imedhihirishwa na azma ya Afrika Kusini na Zimbabwe kukijumuishwa katika mtaala wa elimu katika shule za msingi<sup>1</sup>. (Khumalo 2018)

Ni kweli kwamba fasihi na utamaduni wa Afrika Mashariki huwasilishwa kwa lugha asilia kama vile Kisukuma, Kinyarwanda, Kidinka, Kigisu, na Kitaita au na lugha za Kigeni kama vile Kiingereza na kwa kiasi fulani kwa Kifaransa. Wakazi wa Afrika Mashariki hujifaragua kwa kutunga au kutenda fasihi simulizi na hata andishi na kutekeleza vipengele mbalimbali vya utamaduni wao kwa kutumia hizi lugha asilia au lugha za kigeni. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba kwa sasa hivi hakuna lugha yoyote nyingine ya Afrika Mashariki inayotumika kufumbata hali halisi ya maisha, fasihi na utamaduni wa Afrika Mashariki kama Kiswahili.

Kwa miaka nenda na miaka rudi tahakiki za fasihi na Kiswahili zikiwaandikwa katika majarida ya Kiingereza au labda Kifaransa. Hata jarida hili la EACLS limekuwa linatumia lugha ya Kiingereza katika kuchapisha makala ambazo huzungumzia na kutathmini fasihi na utamaduni wa Afrika Mashariki ambao aghalabu huwasilishwa na kujipambanua kwa lugha asilia zisizokuwa lugha hizo za kigeni.

---

<sup>1</sup>Vituo mbalimbali vya kimataifa vya redio na runinga vimekuwa na mazoea ya kurushwa matangazo katika lugha hii ya mawasiliano mapana Afrika Mashariki. Katika orodha ifuatayo kuna vile vituo vinaendelea au vilivyowahi kurusha matangazo kwa Kiswahili: Idhaa ya Kiswahili ya BBC; Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Ujerumani, DW; Radio Japan; China Radio; All India Radio; Radio Moscow; Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Amerika, VOA; Radio Channel Afrika, Ghana Broadcasting Corporation, n.k.

Hatuna haja kujitosa katika mdahalo wa kama Kiswahili ni lugha asilia au ngeni au kama ipo kati kwa kati baina ya uasilia na ugeni. Itoshe hapa kusema kwamba lugha hii ambayo baadhi ya wataalamu wanasema ni lugha chotara kati ya lugha za Kibantu na Kiarabu na wengine wanasema ni lugha ya Kibantu asilia, ndiyo *lingua franca* ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo ni jambo mwafaka kwamba itumike pia katika kutathmini fasihi na utamaduni wa watu wa Afrika Mashariki. Tunatambua mchango wa majarida na machapisho ambayo yametangulia kuzipa fursa tahakiki zilizoandikwa kwa Kiswahili na tunawapa mkono wa tahania wahariri na wakurugenzi waliong'amua umuhimu wa hatua hiyo. Kwa toleo hili mahsusi la Kiswahili nasi twajitosa katika kina cha bahari pana ya uchapishaji wa makala za Kiswahili ili kutoa mchango wetu na kutoa fursa kwa wahakiki kutumia lugha hii faridi katika hamkani zao.

Wahakiki waliochangia makala katika toleo hili wametumia Kiswahili kuwasilisha tathmini yao ya vipengele mbalimbali vya fasihi na utamaduni wa Afrika Mashariki chini ya kile tulichoamua kukiita mwavuli wa 'mielekeo mipya katika fasihi ya Kiswahili.' Tunaelewa fika kwamba suala la upya ni la mjadala mpana na wa kina. Hapo sipo pahali pa kuliongelea kwa mapema na marefu. Ila ni dhahiri shahiri kwamba upya wa mielekeo wanaoungazia umo zaidi ya ukweli kwamba ndio mara ya kwanza jarida hili kuhitari kutumia Kiswahili. Upya umo katika mikabala na mitindo ya kifasihi inayofumbatwa na wasanii wa ukanda wa Afrika Mashariki. Upya pia unaweza kupatikana katika mikabala ya kihakiki inayoandamwa na wahakiki. Hilo la upya wa mikabala ya kihakiki huenda likawa sio jambo linalostahiki kupewa kipaumbele katika utangulizi huu. Muhimu kudokeza hapa kwamba wahakiki waliochangia makala wametuelekeza katika kila kinachoelekea kuwa mielekeo mipya katika fasihi ya Kiswahili inavyojidhihirisha. Mathalan makala ya Ahmad Kipacha kuhusu ushairi msemele anaangazia ubidaa au upya wa misemo anayotumia Euphrase Kezilahabi katika mtindo wake wa kishairi, naye Michael Gromov anamulikia kurunzi yake "riwaya mpya" ya Kiswahili na kubainisha upya wa kimtindo na kifalftsafa kama sio wa kimaudhui. Kwa upande mwingine Angelus Mnenuka anarejelea uwanda mpya kabisa pale anapoangazia "utendajipepe wa fasihi simulizi" huku Evans Makhulo akichanganua nyimbo za msanii maarufu wa Tanzania Mrisho Mpotu.

Ilmuradi tahakiki zilizomo humu zinaashiria wimbi la upya linalovuma katika bahari ya fasihi na utamaduni wa kisanii katika ukanda wa Afrika Mashariki. Tunatumaini kwamba kwa kuzijumuisha tahakiki hizi katika toleo mahsusi la Kiswahili la jarida hili, tumefungua milango mingine ya upya, upya utakaosaidia kuendelea kukiweka Kiswahili mbele na peupe katika ramani ya dunia. Imekuwa fahari yangu kupata fursa ya kuwa mhariri mgeni wa toleo hili la kwanza la jarida hili katika Kiswahili alichokinasibisha Shaaban bin Robert na titi la mama litamu. Itakuwa furaha ilioje kuendelea kuona matoleo mengine ya Kiswahili ya jarida hili azazi!

## Marejeleo

Khumalo, Thomas. "South African Schools to teach Kiswahili from 2020." VOAnews. <https://www.voanews.com/a/south-african-schools-to-teach-kiswahili/4598340.html> downloaded March 4, 2020

Robert, Shaaban bin. *Pambo la Lugha*. Nairobi: Oxford University Press.